# Les prophètes de Dieu

Par Andrea Muñoz Spannaus
*Deuxième conseillère dans la présidence générale des Jeunes Filles*

# Manabii wa Mungu

Na Dada Andrea Muñoz Spannaus
*Mshauri wa Pili katika Urais Mkuu wa Wasichana*

Conférence générale d'octobre 2025

---

*Pour nous saisir de toute bonne chose jusqu'à la Seconde Venue, il est essentiel d'écouter la voix du prophète et d'y obéir.*

Chers jeunes, nous assistons à une merveilleuse session de la conférence générale ! Nous avons déjà entendu trois apôtres vivants de Jésus-Christ. Quelle merveilleuse bénédiction ! Et nous en entendrons un de plus, Henry B. Eyring. Le festin spirituel continue !

Dans mon discours de l'année dernière, j'ai utilisé l'expérience de David et Goliath pour enseigner comment affronter ce monde. Vous souvenez-vous des cinq pierres ? Aujourd'hui, je vais vous parler d'une histoire de l'Ancien Testament que j'ai lue quand j'avais votre âge et dont j'admirais la protagoniste à laquelle je voulais ressembler. La Bible ne nous dit pas son nom. Nous l'appellerons donc « la femme de Sunem », du nom de la ville où elle habitait.

Les Écritures nous disent qu'un jour où Élisée passait par Sunem, « il y avait là une femme de distinction, qui le pressa d'accepter à manger. Et toutes les fois qu'il passait, il se rendait chez elle pour manger». J'imagine que le prophète Élisée était ravi de l'invitation de cette femme à manger chez elle ! Il était déjà venu plusieurs fois quand, un jour, elle dit à son mari : « Voici, maintenant, je perçois que cet homme […] est un saint homme de Dieu. »

La femme dit «Maintenant,je perçois ». Il semble qu'elle ait invité Élisée chez elle sans savoir qu'il était un prophète de Dieu, et qu'elle ait reçu un témoignage par le Saint-Esprit en écoutant attentivement ce que disait et enseignait Élisée. (Souvenez-vous qu'il n'y avait pas

*Kuisikiliza na kuitii sauti ya nabii ni muhimu kwenye kushikilia kila kitu kizuri hadi Ujio wa Pili.*

Wapendwa vijana, ni kikao cha kupendeza cha mkutano wakati huu! Tayari tumewasikia Mitume hai watatu wa Yesu Kristo. Ni baraka kuu iliyoje! Na tutamsikia mmoja mwingine, Mzee Henry B. Eyring. Karamu ya kiroho inaendelea!

Nilipozungumza mwaka uliopita, tulijifunza jinsi ya kuukabili ulimwengu huu kupitia uzoefu wa Daudi kwa Goliati. Mnakumbuka yale mawe matano? Leo ninashiriki hadithi ya Agano la Kale niliyoisoma nikiwa na umri kama wenu, ambayo iliniacha nikitamani kuwa kama mhusika wake. Biblia haituambii jina lake, hivyo tutamwita mwanamke wa Shunemu kwa sababu hili ni jina la mji anakotoka.

Siku moja, nabii Elisha alikuwa akipita Shunemu, na tunasoma kwamba palikuwepo "mwanamke mmoja mwenye cheo; naye [akamwalika]nabii aje ale chakula. Ikawa kila alipopita njia ile, huingia … kula chakula."Nadhani nabii Elisha alikuwa na furaha sana kwa mwaliko wa kula katika nyumba ya yake! Alikuwa tayari amekwenda mara kadhaa wakati siku moja mwanamke alipomwambia mumewe, "Tazama, mimi naona ya kuwa mtu huyuni mtu mtakatifu wa Mungu..

Mwanamke anasema, "Sasa,ninaona." Inaonekana alimwalika Elisha nyumbani kwake bila kujua alikuwa nabii; alipokea ushuhuda wake kupitia Roho Mtakatifu kwa kusikiliza kwa makini kile Elisha alichofanya na kufundisha. (Kumbukeni, hakukuwa na picha kipindi hicho!

de photos à cette époque ! Il était donc difficile de reconnaître le prophète uniquement à son visage.)

Mais l'histoire ne s'arrête pas là. Un jour, la femme dit à son mari : « Faisons une petite chambre haute […] et mettons-y pour lui un lit, une table, un siège et un chandelier, afin qu'il s'y retire quand il viendra chez nous. »

Cette femme fidèle était disposée à construire une chambre dans sa maison pour que le prophète ait un endroit où loger quand il viendrait dans leur ville !

Aujourd'hui, cette expérience nous enseigne une leçon puissante.

Le Seigneur a témoigné à la femme de Sunem qu'Élisée était un prophète de Dieu et elle a ouvert sa maison pour l'accueillir.

Nous pouvons, nous aussi, recevoir untémoignage personnel des prophètes moderneset ouvrir notre cœur et notre esprit — notre maison — au message que notre Père céleste veut nous transmettre en ces derniers jours.

Chers jeunes, je vous invite à vous poser cette question : Ai-je un témoignage personnel des prophètes vivants ?

Commençons par le commencement.

Qu'est-ce qu'un prophète ?Un prophète est une personne appelée par Dieu pour parler en son nom. Il y a des prophètes sur terre aujourd'hui, tout comme il y en avait dans les temps anciens.

Prophètes, voyants et révélateurs.Cela signifie qu'ils voient ce que les autres ne peuvent pas voir et qu'ils peuvent prophétiser au sujet d'événements futurs. Ils peuvent aussi nous préparer en vue de calamités à venir. Les prophètes reçoivent des commandements et des révélations du Seigneur. Leneuvième article de foiparle de la révélation continue dans les derniers jours, en ces termes : « Nous croyons tout ce que Dieu a révélé, tout ce qu'il révèle maintenant, et nous croyons qu'il révélera encore beaucoup de choses grandes et importantes concernant le royaume de Dieu. »

Gary E. Stevenson a dit : « Le Seigneur continue de révéler ses commandements et sa volonté à ses prophètes, car il désire nous guider vers la joie dans cette vie et la gloire céleste dans la vie à venir. »

Les prophètes proclament aussi l'Évangile, et

Hivyo ilikuwa vigumu kumtambua nabii kwa sura yake.)

Lakini hadithi haikomei hapo. Siku moja, mwanamke akamwambia mumewe, "Tumfanyie chumba kidogo … na ndani yake tumwekee kitanda, na meza, na kiti, na kinara cha taa; na itakuwa, atujiapo, ataingia humo."

Mwanamke huyu mwaminifu alikuwa radhi kutengeneza chumba ndani ya nyumba yake ili kwamba nabii, akipita katika mji, angepata mahala pa kuishi!

Leo tunaweza kujifunza somo lenye nguvu kutokana na uzoefu huu.

Bwana alishuhudia kwa mwanamke wa Shunemu kwamba Elisha alikuwa nabii wa Mungu, na alitenda kwa kuifungua nyumba yake ili kumpokea.

Sisi pia tunaweza kupokeaushuhuda binafsi wa manabii wa Mungu leona kuifungua mioyo yetu na akili zetu—nyumba yetu—kwa ujumbe ambao Baba yetu wa Mbinguni anao kwa ajili yetu katika siku hizi za mwisho.

Wapendwa vijana, ninawaalika mjiulize swali hili: Je, nina ushuhuda binafsi wa manabii wa Mungu walio hai?

Hebu tuanzie mwanzoni.

Nabii ni nani?Nabii ni mtu ambaye Mungu amemwita azungumze kwa niaba Yake.Wapo manabii duniani leo, kama vile ilivyokuwa katika nyakati za kale.

Manabii ni waonaji na wafunuzi.Hiyo humaanisha wanaweza kuona kile wengine wasichoweza kukiona, na wanaweza kutoa unabii wa matukio yajayo. Wanaweza pia kutuandaa dhidi ya majanga. Manabii hupokea amri na mafunuo kutoka kwa Bwana.Makala ya imani ya tisainazungumza juu ya ufunuo unaoendelea katika siku hizi za mwisho. Inasema, "Tunaamini yale yote Mungu aliyoyafunua, na ambayo sasa anayafunua, na tunaamini kwamba bado Yeye atayafunua mambo mengi makuu na muhimu yahusuyo Ufalme wa Mungu."

Mzee Gary E. Stevenson alisema, "Bwana anaendelea kufunua amri Zake na mapenzi yake kwa manabii Wake leo kwa sababu Yeye anatamani kutuongoza kwenye furaha katika maisha haya na kwenye utukufu wa selestia katika maisha yajayo."

Manabii pia huitangaza injili na ni walimu

sont des instructeurs et des messagers inspirés de Dieu pour chaque personne sur terre.

Chacun des membres de la Première Présidence et du Collège des douze apôtres est un prophète, voyant et révélateur. Sous la direction du Seigneur, ils forment un conseil pourvu de l'autorité de déclarer et d'interpréter la doctrine, et de définir les règles de son Église. Ils prient et délibèrent avec attention, car les décisions de ces collèges doivent être unanimes. De cette façon, le Seigneur nous assure que sa volonté sera accomplie.

Les prophètes témoignent du Christ, de son existence, de son ministère et de sa divinité.

Lisons ensemble quelques témoignages de prophètes du Livre de Mormon.

Abinadi a proclamé :

« Dieu lui-même descendra parmi les enfants des hommes et rachètera son peuple.

« Et parce qu'il demeure dans la chair, il sera appelé le Fils de Dieu. »

Samuel le Lamanite a également témoigné que Jésus-Christ est « le Fils de Dieu, le Père du ciel et de la terre, le Créateur de tout depuis le commencement».

Et le prophète Moroni a déclaré : « J'ai vu Jésus, et […] il a parlé face à face avec moi. »

Quand le Sauveur Jésus-Christ est venu sur la terre, l'une des premières choses qu'il a faites a été d'appeler douze apôtres. Il a dit au peuple : «Bénisêtes-vous si vousprêtez attentionaux paroles de ces douze que j'ai choisis. »

J'aimerais maintenant m'adresser aux parents ou aux autres membres de la famille qui élèvent des enfants. Le Seigneur lui-même a enseigné les vérités du plan du salut à Adam et Ève. Il leur a ensuite dit : « Je vous donne le commandementd'enseigner libéralementces choses à vos enfants. »

Que signifie « enseigner libéralement » ? Cela signifie apprendre les vérités de l'Évangile, avoir un témoignage personnel de ces vérités et les transmettre à nos enfants. Cela signifie rechercher les occasions formelles et informelles de les instruire. Cela veut dire mener une vie conforme à cette connaissance et ce témoignage.

Le Livre de Mormon décrit les 2 060jeunes guerriers comme « des hommes pleins de vérité et de sérieux,car on leur avait enseignéà garder les commandements de Dieu et à marcher en droiture devant lui». Ces jeunes guerriers obéissaient fidèlement à Hélaman, qui était alors leur

wenye uvuvio na wajumbe wa Mungu kwa kila mmoja duniani.

Kila mshiriki wa Urais wa Kwanza na Akidi ya Mitume Kumi na Wawili ni nabii, mwonaji, na mfunuzi.Wakihudumu kama baraza chini ya maelekezo ya Bwana, wana mamlaka ya kutangaza na kufafanua mafundisho na kuweka sera kwa ajili ya Kanisa Lake.Kwa makini wanasali na kufanya shauri, kwani maamuzi ya akidi hizi lazima yatolewe kwa kauli moja. Kwa njia hii, Bwana anatuhakikishia kwamba mapenzi Yake yatatendeka.

Manabii wanashuhudia kumhusu Kristo—uwepo Wake, huduma Yake, na utakatifu Wake.

Ngoja tusome baadhi ya shuhuda za manabii ndani ya Kitabu cha Mormoni.

Abinadi alitangaza:

"Mungu mwenyewe atashuka miongoni mwa watoto wa watu, na atawakomboa watu wake.

"Na kwa sababu anaishi katika mwili ataitwa Mwana wa Mungu."

Samweli Mlamani pia alishuhudia kwamba Yesu Kristo ni "Mwana wa Mungu, Baba wa mbingu na dunia, Muumba wa vitu vyote tangu mwanzo."

Na nabii Moroni alisema, "Nimemuona Yesu, na … amenizungumzia uso kwa uso."

Wakati Kristo alipowatembelea Wanefi, moja ya vitu vya mwanzo Yeye alivyofanya ilikuwa kuwaita Mitume kumi na wawili.Naye akawaambia watu, "Heriikiwamtasikilizamaneno ya hawa kumi na wawili ambao nimewachagua."

Sasa, ngoja nishiriki maneno machache kwa wazazi au wanafamilia wengine wanaowalea watoto. Bwana mwenyewe aliwafundisha Adamu na Hawa kweli za mpango wa wokovu. Na kisha aliwaambia, "Ninakupeni amri,kuyafundisha mambo haya kwa uhurukwa watoto wenu."

Inamaanisha nini kufundisha kwa uhuru? Ni kujifunza kweli za injili, kuwa na ushuhuda binafsi wa kweli hizo, na kushiriki maarifa hayo kwa watoto wetu.Ni kuhimiza vyote, nyakati rasmi na zisizo rasmi za kufundisha.Ni kuishi kulingana na maarifa na ushuhuda huo.

Kitabu cha Mormoni kinawaelezea vijana mashujaa2,060 kama "watu wa ukweli na wenye busara, kwaniwalikuwa wamefundishwakutii amri za Mungu na kutembea wima mbele yake."-Wavulana hawa kwa uaminifu walimtii Helamani, ambaye kwa wakati huo alikuwa kiongozi

chef de guerre et leur prophète, et ils rendaient hommage à leurs mères, qui leur avaient inculqué des principes de vérité et de foi.

Chers parents, dans ce monde où tant de voix différentes s'opposent et où les ténèbres règnent parfois, Dieu nous a commandé d'élever nos enfants dansla lumière et la vérité. Il nous a confié la responsabilité d'enseigner à nos enfants les vérités salvatrices de l'Évangile. Si nous ne le faisons pas, ce n'est pas le monde qui le fera.

Chers jeunes amis, j'aimerais vous lancer une invitation : Dans les jours à venir, je vous invite à vous agenouiller, à ouvrir votre cœur et à demander avec foi à notre Père céleste qu'il vous donne la confirmation que le prophète et les douze apôtres qu'il a choisis sont ses porte-parole sur la terre aujourd'hui.

La femme de Sunem nous a montré que le Saint-Esprit peut nous donner ce témoignage. Je vous promets que, en dépit de nos difficultés continues, la vie est plus facilequand noussavonsque ces hommes ont été choisis par Dieu, car nous suivons leurs conseils avec confiance, foi et espoir. Pour noussaisir de toute bonne chosejusqu'à la seconde venue de notre Sauveur, il est essentiel d'écouter la voix du prophète et d'y obéir.

La méchanceté du monde ne cesse de croître, mais l'Église de Jésus-Christ et son royaume sont plus forts que jamais. Sion revêt ses habits de fêteet le trône du Christ ne sera pas ébranlé. Le Seigneur attend de nous que nous soyons forts dans notre témoignage, pleins de foi, et que nous nous repentions quotidiennement. Notre Sauveur, Jésus-Christ, compte sur chacun de nous pour faire avancer son œuvre.

Joseph Smith, le prophète, a déclaré un jour : « Frères, ne persévérerons-nous pas dans une si grande cause ? » Cependant, comme mon message s'adresse principalement à vous, les jeunes, j'aimerais remplacer le termefrèrespar le motjeunes. Êtes-vous prêts ?

« Chers [jeunes], nepersévérerons-nous pas dans une si grande cause ?Allez de l'avantet pas en arrière.Courage,chers [jeunes] ; et en avant,en avant, vers la victoire! Que votre cœur se réjouisse etsoit dans l'allégresse. »

Je suis reconnaissante pour les directives et les efforts consacrés des prophètes vivants. Je vous rends solennellement témoignage qu'ils sont appelés de Dieu à établir, à faire avancer et à diriger son royaume sur terre aujourd'hui. Et il en sera toujours ainsi ! Ce sera toujours le

wao wa jeshi na pia nabii wao, na walitambua kwamba mama zao walikuwa wameijaza mioyo yao kwa ukweli na imani.

Wazazi, katika ulimwengu huu ambapo kuna sauti nyingi na nyakati zingine kiza kinene, Mungu mwenyewe ametuamuru kuwalea watoto wetu katikanuru na kweli.Ametuamini kwa jukumu la kuwafundisha watoto wetu kweli za kuokoa za injili. Ikiwa tutashindwa kufanya hivyo, ulimwengu hautabeba jukumu hilo.

Wapendwa marafiki vijana, nina mwaliko kwa ajili yenu: Katika siku zinazokuja, ninawaalika mpige magoti, mfungue mioyo yenu, na msali kwa imani kwa Baba wa Mbinguni mkimuomba awathibitishie kwamba nabii na mitume Wake ni sauti Yake duniani leo.

Mwanamke Mshunami ametufunza kwamba tunaweza kuwa na ushuhuda huo kupitia Roho Mtakatifu. Ninawaahidi kwamba paletunapojuakwamba wao ni wapakwa mafuta wa Mungu, maisha yetu yatakuwa rahisi licha ya changamoto zinazoendelea,kwani tutatii sauti yao kwa ujasiri, imani, na tumaini.Kuisikiliza na kuitiisauti ya nabii ni muhimu kwenyekushikilia kila kitu kizurihadi Ujio wa Pili wa Mwokozi wetu.

Uovu wa ulimwengu unaongezeka, lakini Kanisa la Yesu Kristo na ufalme wake ni imara kuliko ilivyowahi kuwa. Sayuni inajivika mavazi yake mazuri,na enzi ya Kristo haitaanguka. Bwana anatutarajia kuwa imara katika shuhuda zetu, kuwa waliojaa imani, na kutubu kila siku. Mwokozi wetu, Yesu Kristo, anamtegemea kila mmoja wetu kuisongesha mbele kazi Yake.

Nabii Joseph Smith aliwahi kusema, "Ndugu, je, si lazima sisi tuendelee katika kazi hii iliyo kuu?" Hata hivyo, kwa kuwa ujumbe wangu ni mahususi kwa ajili yenu, vijana, ningependa kutumia nenovijanabadala yandugu. Mpo tayari?

"[Vijana], je, si lazima sisituendeleekatika kazi hii iliyo kuu?Twende mbelena siyo nyuma.Tuweni majasiri, [vijana]; na mbele,mbele kwenye ushindi!Acheni mioyo yenu ifurahi, nakuwa yenye furaha zaidi."

Nina shukrani kwa mwongozo na juhudi zilizowekwa wakfu za manabii walio hai. Ninatoa ushuhuda wangu wa unyenyekevu kwamba, waliitwa na Mungu ili kuendeleza, kuanzisha, na kuongoza ufalme wake duniani leo.Na itakuwa hivyo daima. Daima itakuwa kwamba Bwana

Seigneur qui choisira ses serviteurs. Au nom de Jésus-Christ. Amen.

anawachagua watumishi Wake.Katika jina la Yesu Kristo, amina.